

KUMB: PPR/18 - 03/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUENZIA JUMATANO, TAREHE 7 MACHI 2018

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 7 Machi 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Februari 2018. Kwa mwezi Machi 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 1/lita (sawa na asilimia 0.06), Shilingi 69/lita (sawa na asilimia 3.37) na Shilingi 4/lita (sawa na asilimia 0.20) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 1/lita (sawa na asilimia 0.06), Shilingi 69.50/lita (sawa na asilimia 3.56) na Shilingi 4.17/lita (sawa na asilimia 0.21) sawia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani limetokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premium*) na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini hazijabadilika kwa sababu hakuna mzigo mpya wa mafuta uliopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Februari 2018. Hivyo, bei za mafuta katika Mikoa ya Kaskazini kwa mwezi wa Machi 2018 zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa katika mwezi wa Februari 2018.
- (c) Ifahamike kwamba, katika shehena sita za mafuta zilizopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam katika mwezi Februari 2018, tano zilinunuliwa kwa bei za soko la dunia za mwezi Disemba 2017 na moja ilinunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Januari 2018.
- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017**.**
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni

zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,227	2,134	2,059
Arusha	2,278	2,163	1,995
Arumeru (Usa West)	2,278	2,163	1,995
Karatu	2,297	2,181	2,013
Monduli	2,284	2,168	2,000
Monduli-Makuyuni	2,288	2,173	2,005
Ngorongoro (Loliondo)	2,363	2,247	2,079
Kibaha	2,232	2,139	2,063
Bagamoyo	2,238	2,145	2,070
Kisarawe	2,234	2,141	2,066
Mkuranga	2,237	2,144	2,069
Rufiji	2,255	2,162	2,086
Dodoma	2,286	2,193	2,118
Bahi	2,293	2,200	2,125
Chemba	2,312	2,219	2,144
Kondoa	2,319	2,225	2,150
Kongwa	2,283	2,190	2,115
Mpwapa	2,287	2,194	2,119
Iringa	2,291	2,198	2,123
Kilolo	2,296	2,202	2,127
Mufindi (Mafinga)	2,301	2,208	2,133
Njombe	2,319	2,226	2,151
Njombe (Kidegembye)	2,340	2,247	2,172
Ludewa	2,357	2,264	2,189
Makete	2,350	2,257	2,182
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,317	2,224	2,149
Bukoba	2,442	2,349	2,274
Biharamulo	2,417	2,323	2,248
Karagwe (Kayanga)	2,459	2,365	2,290

Kyerwa (Ruberwa)	2,464	2,371	2,296
Muleba	2,442	2,349	2,274
Ngara	2,408	2,315	2,239
Misenyi	2,451	2,357	2,282
Geita	2,392	2,299	2,224
Bukombe	2,381	2,288	2,213
Chato	2,413	2,320	2,245
Mbogwe	2,430	2,337	2,262
Nyang'hwale	2,407	2,314	2,239
Kigoma	2,458	2,365	2,290
Uvinza (Lugufu)	2,470	2,377	2,302
Buhigwe	2,447	2,354	2,279
Kakonko	2,415	2,322	2,247
Kasulu	2,444	2,351	2,276
Kibondo	2,422	2,329	2,254
Moshi	2,268	2,152	1,984
Hai (Bomang'ombe)	2,271	2,156	1,988
Mwanga	2,261	2,145	1,977
Rombo (Mkuu)	2,285	2,169	2,001
Same	2,254	2,139	1,971
Siha (Sanya Juu)	2,274	2,159	1,991
Lindi	2,286	2,193	2,118
Lindi-Mtama	2,304	2,211	2,136
Kilwa Masoko	2,261	2,168	2,093
Liwale	2,307	2,214	2,139
Nachingwea	2,315	2,222	2,147
Ruangwa	2,317	2,224	2,148
Babati	2,312	2,197	2,029
Hanang (Katesh)	2,323	2,207	2,039
Kiteto (Kibaya)	2,328	2,212	2,044
Mbulu	2,325	2,209	2,041
Simanjiro (Orkasumet)	2,344	2,229	2,061
Musoma	2,405	2,312	2,237
Musoma Vijijini (Busekela)	2,446	2,353	2,278
Rorya (Ingirijuu)	2,414	2,321	2,246
Rorya (Shirati)	2,449	2,356	2,281
Bunda	2,397	2,303	2,228
Butiama	2,402	2,309	2,234
Serengeti (Mugumu)	2,451	2,358	2,283
Tarime	2,416	2,323	2,248
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,421	2,328	2,253
Mbeya	2,334	2,241	2,166
Chunya	2,344	2,250	2,175
Chunya (Makongolosi)	2,358	2,265	2,189
Ileje	2,347	2,254	2,179
Kyela	2,350	2,257	2,182
Mbarali (Rujewa)	2,318	2,225	2,150
Mbozi (Vwawa)	2,343	2,250	2,175

Momba (Chitete)	2,352	2,259	2,184
Rungwe (Tukuyu)	2,343	2,250	2,175
Morogoro	2,252	2,159	2,084
Mikumi	2,268	2,175	2,099
Kilombero (Ifakara)	2,290	2,197	2,122
Kilombero (Mlimba)	2,312	2,219	2,144
Kilombero (Mngeta)	2,302	2,208	2,133
Ulanga (Mahenge)	2,301	2,207	2,132
Malinyi	2,311	2,218	2,142
Kilosa	2,271	2,177	2,102
Gairo	2,271	2,177	2,102
Mvomero (Wami Sokoine)	2,263	2,169	2,094
Turiani	2,277	2,184	2,109
Mtwara	2,300	2,206	2,131
Nanyumbu (Mangaka)	2,348	2,255	2,180
Masasi	2,325	2,232	2,157
Newala	2,332	2,238	2,163
Tandahimba	2,325	2,231	2,156
Mwanza	2,377	2,284	2,209
Kwimba	2,413	2,320	2,245
Magu	2,385	2,292	2,217
Misungwi	2,383	2,289	2,214
Sengerema	2,409	2,316	2,241
Ukerewe	2,436	2,343	2,268
Sumbawanga	2,400	2,307	2,231
Kalambo (Matai)	2,407	2,314	2,239
Nkasi (Namanye)	2,413	2,320	2,245
Katavi (Mpanda)	2,435	2,342	2,266
Mlele (Inyonga)	2,413	2,320	2,245
Songea	2,350	2,257	2,182
Mbinga	2,384	2,291	2,216
Namtumbo	2,380	2,286	2,211
Nyasa (Mbamba Bay)	2,386	2,293	2,218
Tunduru	2,409	2,316	2,241
Shinyanga	2,356	2,263	2,187
Kahama	2,370	2,276	2,201
Kishapu	2,384	2,291	2,216
Simiyu (Bariadi)	2,397	2,304	2,229
Busega (Nyashimo)	2,390	2,297	2,222
Itilima (Lagangabilili)	2,400	2,307	2,232
Maswa	2,389	2,295	2,220
Meatu (Mwanhuji)	2,396	2,303	2,227
Singida	2,318	2,225	2,149
Iramba	2,330	2,237	2,161
Manyoni	2,302	2,209	2,134
Ikungi	2,313	2,220	2,145
Mkalama (Nduguti)	2,342	2,249	2,174
Tabora	2,381	2,288	2,213

Igunga	2,335	2,242	2,167
Kaliua	2,399	2,306	2,231
Ulyankulu	2,393	2,300	2,225
Nzega	2,346	2,253	2,177
Sikonge	2,393	2,300	2,225
Urambo	2,394	2,301	2,226
Tanga	2,222	2,106	1,938
Handeni	2,242	2,127	1,959
Kilindi	2,257	2,142	1,974
Korogwe	2,234	2,118	1,950
Lushoto	2,243	2,128	1,960
Mkinga (Maramba)	2,229	2,113	1,945
Muheza	2,227	2,111	1,943
Pangani	2,228	2,113	1,945

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,116.34	2,023.10	1,947.92

Bei za Jumla – TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,110.83	1,995.12	1,827.17

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA